# HOTUBA YA MGENI RASMI DR.SALIM AHMED SALIM MWENYEKITI TAASISI YA MWALIMU NYERERE

## WAKATI WA

**CHAKULA CHA HISANI KILICHOANDALIWA KWA AJILI YA KUCHANGISHA FEDHA ZA UKARABATI WA MAJENGO, VIFAA NA HUDUMA NYINGINEZO**

**KATIKA SHULE YA MTAKATIFU YOSEFU**

***Dar es salaam, Mei 3,* 2002**

Mwadhama Polycarp Kadinali Pengo, Askofu Mkuu wa
Jimbo kuu la Dar es Salaam

Mhashamu Askofu Method Kilaini, Askofu Msaidizi,
Jimbo kuu la Dar es Salaam

Mheshimiwa Joseph Mungai(MB), Waziri wa Elimu na
Utamaduni

Waheshimiwa Mawaziri

Waheshmiwa Mabalozi

Wageni Waalikwa

Mabibi na Mabwana.

Kwanza naomba nikushukuru kwa mwaliko wenu kuwa niwe mgeni rasmi katika hafla hii. Pili naomba niwasilishe pongezi zangu kwako wewe binafsi na kupitia kwako kwa Kamati uliyoiunda ili ikusaidie kubuni mbinu mbalimbali za kutunisha mfuko na kusimamia ukarabati wa shule ya Millenio ya Mtakatifu Yosefu. Ni juhudi zenu za pamoja ndio zimewezesha kutafsiri lililokuwa wazo kiasi cha mwaka mmoja uliopita na sasa kuwa uamuzi hakika kwamba shule ya Millenio ya Mtakatifu Yosefu katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam inaanza mwezi huu wa Mei, 2002.

Millenio hii itashuhudia mabadiliko makubwa sana katika namna binadamu wanavyoendesha mambo. Mazoea yatatoa nafasi kwa utendaji unaoongozwa na sayansi na teknolojia ambayo yenyewe inatawaliwa na

Millenio hii itashuhudia mabadiliko makubwa sana katika namna binadamu wanavyoendesha mambo. Mazoea yatatoa nafasi kwa utendaji unaoongozwa na sayansi na teknolojia ambayo yenyewe inatawaliwa na kasi kubwa ya mabadiliko. Tunalazimika kubadilika ili twende na mkondo huu wa mageuzi makubwa yanayoendelea duniani ilhali hakuna kisichobadilika bali mabadiliko yenyewe. Jambo kubwa lililo muhimu katika mazingira haya, mazingira ya mageuzi makubwa yasiyokifani na yasiyoepukika, ni kuhakikishia uwezo wetu wa kuyaelewa na kushika hatamu za kuyaongoza tukichuja yale yaliyo mema na ya kheri kwetu na kujiepusha na yale yanayoashiria kutupeleka katika matatizo. Na hakuna nyenzo nyingine yeyote kubwa zaidi itakayotuwezesha kupambana na changamoto na matatizo ya utandawazi kuliko elimu.

Mwadhama Kadinali Pengo,

Umuhimu wa elimu kwa watu wetu ni jambo lililo dhahiri. Elimu imefananishwa na ufunguo wa maisha ya binadamu. Ni imani yangu kwamba elimu ni muhimu katika maisha ni ukweli ambao hauhitaji kusisitizwa mbele ya wageni waliohudhuria hapa jioni ya leo. Hapana shaka hata uamuzi wao kuwa nasi umezingatia pamoja na sifa nyingine kuwa ni waumini wa dhana kuwa elimu ni ufunguo wa maisha. Sifa nyingine ni

ukarimu wa mioyo yetu kuweza kuchangia na kuwaongezea nguvu wale waliokabidhiwa jukumu la kukamilisha ukarabati wa majengo ya shule ikiwa ni pamoja na kuweza kuweka mazingira ya shule yafanane na shule iliyokusudiwa ya Millenio ya tatu.

Uwezo wa kuchangia unahitilafiana. Kubwa ni kwamba tunakubaliana juu ya jambo tunaloombwa kuchangia:- Yaani ELIMU BORA KWA WATOTO WETU. Wapo miongoni mwetu ambao wako tayari kujinyima kile kidogo walichonacho ili wawakabidhi watoto wao ufunguo wenye uhakika katika maisha yaani elimu bora na ya kisasa. Wakati fursa zilikuwa adimu hapa nchini baadhi ya wazazi wamehangaika kutafuta fursa hiyo nje ya nchi. Kuanzishwa kwa shule hii ya Millenio ya Mtakatifu Yosefu kunapanua fursa kwa wazazi kuwasomesha watoto wao, wapate elimu bora zaidi, na katika mazingira ya Kitanzania.

Kwangu mimi elimu bora ni ile inayomwezesha yule anayeipata kuyaelewa na kuyamudu vyema mazingira yanayomzunguka. Katika kila ngazi elimu haina budi kumuongezea binadamu kiwango fulani cha uhuru kwa kumkomboa kutoka hali ya kuwa mtumwa wa mazingira na badala yake imuongezee uwezo wa kuyatawala na kuyageuza kuwa nyenzo ya kujiletea maendeleo. Kwa tafsiri hii kigezo cha jumla cha ubora

wa elimu ni kiasi ambacho elimu hiyo inatuongezea uwezo wa kujitagemea katika mawazo, kauli na matendo yetu.

Ni katika maana hii ndipo usemi wa elimu kuwa ni ufunguo wa maisha hupata maana. Kiwango hiki cha ubora wa elimu humwezesha aliyeipata atambue haki zake katika jamii na vilevile wajibu wake kwa jamii hiyo.

Lakini elimu ni zaidi ya ufunguo wa maisha. Tunayo mifano tele katika dunia inayotuthibitishia kuwa elimu kwa hakika ni ufunguo wa maendeleo kwa jamii. Kiwango cha elimu katika nchi hutofautisha nchi moja na nyingine katika kuyamudu maendeleo. Haishangazi kwamba nchi zinazoitwa zimeendelea ni zile ambazo zimefanikiwa kuwekeza katika kusomesha watu wake. Japan haina raslimali kubwa ukilinganisha na baadhi ya nchi katika bara letu. Lakini imeweza kupiga hatua kubwa ya maendeleo kutokana na uamuzi wa makusudi wa kuwekeza katika elimu kwa watu wake (yaani Human Resource Development).

Siku hizi hatuchoki kusikia mifano ikitolewa ya miujiza iliyofanywa na nchi za Kusini Mashariki mwa bara la Asia na hususani Singapore, Korea Kusini, Indonesia na Malaysia. Maendeleo katika nchi hizi hayakupatikana kwa muujiza mwingine wowote

isipokuwa kwa kuwekeza katika elimu bora kwa watu wake. Ni kweli watu ni raslimali kubwa ya maendeleo lakini watu wenye upeo mkubwa wa dunia kutokana na elimu bora waliyonayo ni raslimali ya uhakika zaidi katika kuleta maendeleo ya kweli katika mazingira ya Millenio hii.

Afrika ni bara la nchi zinazoendelea na ambalo bado ni bara maskini kwa kila kigezo. Lakini kikwazo si uduni wa raslimali bali kiwango cha chini cha elimu kwa idadi ya watu wa bara hili. Ipo haja ya kulitambua hili na tukapania kujifunza vyema kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika nchi za mashariki ya mbali. Lakini jukumu hasa ni la nani ? Ni rahisi kulitupia serikali jukumu lote nasi tukajikosha uwajibikaji. Mtizamo huu si sahihi ingawa katika nchi maskini kama yetu serikali inawajibu mkubwa katika kuandaa mazingira yatakayowezesha mabadiliko ya msingi kufanyika. Uamuzi wa serikali wa kufikiria sera zake za huko nyuma na hasa kuruhusu mashirika ya dini, Taasisi binafsi na watu binafsi, kuwa washiriki wake katika jitihada za kupanua elimu nchini ni mwelekeo mzuri unaopaswa kuungwa mkono na watu wote wenye mapenzi mema kwa taifa letu.

Lakini tatizo ni kubwa kuliko uwezo wa serikali pekee au katika ushirikiano na madhehebu ya dini na

Taasisi mbali mbali nyinginezo. Jitihada hizi inapaswa ziungwe mkono kwa dhati na wadau wengine na hususan wazazi wenyewe. Ni matumaini yangu kitendo hiki cha kuitana na kuchangishana kwa ajili ya maendeleo ya elimu nchini kitapamba moto na kuzagaa nchi nzima iwe ni katika kukabili uhaba wa vyumba vya madarasa, Nyumba za walimu au madawati na kadhalika.

Ninatoa rai kwa taasisi nyingine pamoja na sekta binafsi katika uchumi wa taifa letu kuliona tatizo la elimu duni kuwa ni kikwazo kwa maendeleo ya haraka ya taifa letu, na sote kwa pamoja tuingie katika vita hii ya kulikomboa taifa letu kwa kuwapatia watoto na vijana wetu elimu bora. Labda niongeze kwa kjusema kwamba kwa kuzingatia ushauri na Busara wa Baba wa Taifa, Taasisi ya Mwalimu Nyerere inatilia mkazo mkubwa umuhimu wa Elimu bora kwa watoto wetu wote.

Mwadhama Kadinali Pengo, Waheshimiwa wageni waalikwa, sasa naomba nimalizie kwa kukupongeza na kukushukuru kwa kauli uliyoitoa kwamba elimu itakayotolewa katika shule tunayoichangia itakuwa kwa watoto wote bila kujali imani zetu tofauti wala rangi wala kabila. Huu ni msimamo sahihi na thabiti unaopaswa kuungwa mkono na kila mmoja wetu. Watoto wa taifa letu waliolelewa katika mazingira yasiyokuwa na ubaguzi

watakuwa chachu katika kudumisha umoja na mshikamano wa taifa letu. Kama walivyoshirikiana na kusaidiana wangali shule malezi haya yatajenga misingi imara ya kuvumiliana na kushirikiana licha ya tofauti zetu.

Mwisho kabisa naomba niungame. Pamoja na haya yote niliyoyasema, nina sababu ya ziada ya kushiriki kwangu katika shughuli hii ya leo. Mke wangu Amne, alikuwa mwanafunzi wa St. Joseph Convent kwa kipindi cha miaka kumi na mbili mfululizo yaani tokea shule ya msingi hadi sekondari (Januari 1951 hadi Desemba, 1963).

Ninakutakieni mafanikio mema na Mwenyezi Mungu azibariki jitihada zenu.

Ninawashukuru kwa kunisikiliza.